GRADE 7 KISWAHILI (INSHA NA UTANGULIZI WA FASIHI)

MARKING SCHEME & TEACHER'S GUIDE

Jumla ya alama: 50

ZOEZI I: INSHA — ALAMA 15

Mada: “Usiku huo nilisikia hodi mlangoni, na nilipoifungua milango, nilikumbana na jambo ambalo sikulitarajia.”

Insha iwe na maneno 300–350. Alama zitolewe kwa kuzingatia maudhui, mpangilio/mtiririko, matumizi ya lugha na usahihi wa sarufi, tahajia na uakifishaji.

Kigezo	Alama	Mwongozo	Utekelezaji
Maudhui na uhusiano na mada	6	Mada imeendelezwa kikamilifu; tukio la kushtukiza limeelezwa kwa maelezo yanayoeleweka.	6 bora; 4–5 vizuri; 2–3 dhaifu; 1 kwa maudhui machache; 0 yasiyohusiana.
Mpangilio na mtiririko	3	Utangulizi, maendeleo na hitimisho vinafuatana kwa mantiki.	3 bora; 2 una mapungufu machache; 1 mtiririko dhaifu; 0 haujapangika.
Msamiati na mtindo	3	Msamiati mwafaka, sentensi zenye utofauti na mtindo unaofaa.	3 bora; 2 wastani; 1 mdogo; 0 duni.
Sarufi, tahajia na uakifishaji	3	Makosa ni machache na hayaathiri maana.	3 makosa machache; 2 baadhi; 1 mengi; 0 makosa mengi yanayozuia maana.

Maelekezo: Usikate alama kwa mtazamo binafsi wa mwalimu kuhusu hadithi. Tathmini insha kwa vigezo vilivyo hapo juu na ukubali majibu tofauti mradi yahusiane na mada.

ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI — ALAMA 20

2(a)(i) — 2

Ujumbe mkuu: umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii katika kilimo, kushughulikia mashamba na kushirikiana ili kuongeza uzalishaji na kuondoa njaa. Alama 2 kwa ujumbe ulio kamili; 1 kwa wazo moja sahihi.

2(a)(ii) — 4

Sifa zozote mbili zenye maelezo: huwasilishwa kwa njia ya kuimbwa/kutendwa; huhifadhiwa na kusambazwa kwa njia ya masimulizi/utendaji; huhusisha ushiriki wa hadhira; huweza kuandamana na mdundo/makofi/ishara. Alama 2 kila sifa iliyoelezwa.

2(a)(iii) — 4

Mbinu zozote mbili pamoja na mifano: uradidi — “Nime...”/“T...” katika mistari; tashbihi au taswira inapofafanuliwa kutoka kwenye wimbo; amri — “Turejee”, “Tutie”, “Tujifunge”, “Udongo tutifue”; matumizi ya kauli za kuhamasisha. Alama 2 kila mbinu: 1 kutaja, 1 mfano/maelezo.

2(a)(iv) — 2

Maadili: bidii, uwajibikaji, ushirikiano, uzalendo/kujitegemea, upendo wa kazi. Alama 1 kila moja.

2(a)(v) — 4

Kauli hiyo ni mwito wa kuhamasisha na kuwatia moyo wasikate tamaa katika kazi ya kilimo. Inaonyesha ushirikiano na bidii. Alama 2 kwa maana; alama 2 kwa umuhimu katika muktadha.

2(a)(vi) — 4

Mambo mawili: kutumia sauti/mdundo unaofaa; kupiga makofi au kutumia ishara za mwili; kuhusisha hadhira kwa kuitikia; kupanga waimbaji katika kundi. Alama 2 kila jambo lililoelezwa.

ZOEZI III: NOVELA — ALAMA 10

3(a) — 2

Mazingira mawili ya wakati: usiku; baada ya Herina kuwasiliana na ndugu/mama yake; kipindi cha baada ya kukumbwa na changamoto ya elimu. Alama 1 kila mazingira yanayokubalika kutoka dondoo.